**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 9 Aprili, 2013**

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

*(Mkutano Ulianza Saa 3.00 Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa msimame tena. Mtakumbuka kwamba wakati wa Vikao vyetu vya Kamati, kwa bahati mbaya sana tulimpoteza mpenzi wetu Mheshimiwa Salim Hemed Khamis. Kwa hiyo, tumkumbuke kwa dakika moja.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa Dakika moja kumkumbuka Mheshimiwa Salim Hemed Khamis aliyekuwa Mbunge wa Chambani*

Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, Amin. Ahsanteni sana na karibuni tukae.

Waheshimiwa Wanbunge, katika Mkutano wa Tisa, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Serikali uitwao *The Plant Breeders` Rights Bill, 2012,* kwa taarifa hii napenda kulialifu Bunge hili Tukufu kwamba, Mswada huo umekwisha pata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria ya nchi iitwayo: *The Plant Breeders` Rights Act, 2012* Na. 9 ya mwaka 2012. Kwa hiyo, ule sasa ni sheria ya Nchi.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kuwasilisha mezani Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

### Kujenga Barabara ya Old Moshi kwa Lami

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI)** aliuliza:-

Je, Serikali itatekeleza lini ahadi ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya *Old Moshi* inayoanzia Kiboriloni kupitia Kikarara, Tsuduni hadi Kidia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika kampeni ya Urais ya mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alifika eneo la Kata ya *Old Moshi* Mashariki na kufanya Mkutano wa Hadhara na wananchi wa eneo hilo ambapo alitoa ahadi ya kujenga Barabara ya *Old Moshi,* kwa maana ya Kiboriloni hadi Kikarara-Tsuduni mpaka Kidia yenye urefu wa kilomita 10.3 kwa kiwangop cha lami.

Barabara hii inapita kwenye maeneo yenye mteremko mkali na mvua nyingi kwa mwaka, hivyo athari za mmomonyoko wa udonhgo ni kubwa kwa wakati wote wa mvua.

Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili iendelee kupitika ikisubiri upatikanaji wa fedha za kuitengeneza kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011 barabara hiyo ilitengewa kiasi cha shilingi milioni 32.76, na mwaka wa fedha wa 2011/2012 shilingi milioni 22 na mwaka wa fedha wa 2012/2013 shilingi milioni 22.48 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 zimetengwa shilingi milioni 48 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida ya barabara hiyo. Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imeshauriwa kuandaa maombi maalum kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa barabara hiyo na hivyo itaendelea kutenga fedha za matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri amekiri mwenyewe kwamba barabara hiyo ya Kikarara-Tsuduni hadi Kidia inapita kwenye miteremko mikali sana, na kwamba kila mwaka Serikali imekuwa inatenga pesa kwa kiwango kidogo kidogo kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha udogo huo huo.

Moja, Waziri haoni kwamba kutenga fedha kidogo kidogo kutengeneza barabara ya miteremko mikali kwa udongo ni kupoteza fedha za Serikali? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Mheshimiwa Rais alipita maeneo mengi sana na kuweka ahadi ya kutengeneza barabara pamoja na Miundombinu ya aina nyingine, ikiwemo na barabara ya kule Kyela Mkoani Mbeya ya Kikyusya mpaka Matema ya kilomita 39.2.

Mpaka leo, barabara hiyo ndiyo imetengenezwa kwa kiwango cha kilomita 2.5. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais katika Miundombinu mbalimbali inatengenezwa mapema ili wananchi kuendelea kuwa na imani na Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godfrey W. Zambi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bajeti ni mpango wa Serikali unaoonyesha jinsi tutakavyopata fedha na namna zitakavyotumika na Bajeti hii tunayoizungumza hapa inaitwa *Cash Budget,* ukisema hizi ni fedha kwa ajili ya vitumbua, unanunua vitumbua! Hizi ni kwa ajili ya maandazi unanunua maandazi. Hizi ni kwa ajili ya maziwa kwa ajili ya watoto unanunua maziwa na fedha hizi tunazipanga kufatana na uwezo wa nchi kwa maana ya uchumi wenyewe.

Nataka niseme kwamba fedha hizi zimekuwa zinatoka kidogo kidogo kwa sababu ya hali halisi, hizi Halmashauri zetu tunaziwekea *ceiling*. Mheshimiwa Zambi yuko katika Kamati hii inayoshughulikia TAMISEMI na wakati wote tumetaka tupandishe, lakini hatukuweza kufanya hivyo kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti wenyewe. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni kweli kabisa kama anavyosema Mheshimiwa Godfrey Zambi, ukitenga fedha hizi kidogo kidogo, unaweza usifikie lengo ambalo umejiwekea. Barabara inayozungumzwa hapa, tume-*check* katika mpango wa serikali wa Mkoa wa Kilimanjaro na tumekuta kwamba barabara hii, imetengewa fedha imewekewa katika mpango huo huo, lakini ndani yake inazungumza habari ya barabara ya changarawe na ndiyo maana tumezungumza sisi hapa na *Engineer* wa Wilaya na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.

Tukamwambia kwamba aweke mpango ambao utaomba maombi maalum kwa Serikali na iletwe hapa Bungeni, ili Serikali iruhusu fedha hizo ziweze kutumika.

Pili, kule Kyela, Mheshimiwa Zambi amezungumza habari ya kilomita 2.5 na pia amezungumzia kuhusu ahadi ambazo zimetolewa na Mheshimiwa Rais. Kila wakati tunapokuja hapa mbele yako Mawaziri wote na sasa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, huwa hatuna Mdahalo wala hatuna habari ya kuzungumzia ahadi ya Rais kwamba itekelezwe au isitekelezwe.

Ahadi ya Rais ikishatoka, sisi tunachofanya hapa ni kutekeleza ahadi yake, hakuna tena kwenda kukaa tunazungumza, Halmashauri hii ya Kyela ambayo Mheshimiwa anazungumza hapa, sisi tunachotaka kujua ni kujua kama tumeingiza katika mpango huu. Sasa sina *details* zake, namwomba Mheshimwa Zambi anipe nafasi, nitakwenda kukaa na watu wangu tuangalie kwamba imepangiwa mpango gani, lakini nataka niseme, ahadi zote za Rais zilizotolewa ni wajibu wetu sisi kama Serikali kuhakikisha zinatekelezwa. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa nafasi. Kwa kuwa ahadi ni deni na kwa kuwa madeni haya tunayoyazungumzia ni madeni ambayo yanatakiwa kulipwa na Mheshimiwa Rais, na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge ndiyo wafuatiliaji wakuu wa ulipwaji wa madeni haya.

Je, ni lini serikali itaandaa madeni hayo na kama nilivyowahi kuomba, ili madeni hayo yaletwe hapa Bungeni, ili Waheshimiwa Wabunge waweze kujiridhisha namna gani madeni haya yatalipwa kwa sababu Waheshimiwa Wabunge ndiyo ambao watabaki kudaiwa kule kijijini na matokeo yake hakuna Mbunge atakayerudi Bungeni hapa kama madeni haya hayatalipika! Haya madeni ni ya Wabunge, wakati mwingine siyo ya Rais tena. Naomba Serikali ituambiae, lini ahadi hizi zitaletwa hapa ili tuone mpango wake wa kulipwa madeni haya, ni lini na siyo maneno ni lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lugola, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa anavyosema kwamba ahadi ni deni, kwa hapa tunapozungumza hapa lazima useme kwa maneno! Lazima ujibu kwa maneno yaani lazima useme maneno, kwa kule kwenye *field*, lazima ionekane kwa vitendo, kama ni Daraja lionekane lile pale.

Mheshimiwa Spika, mimi naelewa, ….hiyo naielewa kabisa, lazima uonyeshe barabara pale na kila kitu, lakini tunapojibu hapa Bungeni sasa, tunayasema kwa maneno, tunaeleza kwanza kwa maneno ili tukitoka hapa tunakwenda vizuri.

Hii orodha anayoizungumzia Mheshimiwa Lugola na kwa taarifa ya Waheshimiwa Wabunge, orodha hii ilikwisha kutolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Mikoa yote ilitakiwa ilete hapa na orodha ile inafahamika na ndiyo maana nasimama

hapa *with confidence* kukuambia haya ni maelekezo ya Serilkali na Serikali imeagiza kwamba sisi tutekeleze, wala hatuna haja ya kukaa tunabishana hapa, orodha ilishatengezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa sababu mazingira ya barabara ya Kiboriloni hadi Kidia kule katika Jimbo la Moshi Vijijini inafanana sana na mazingira ya barabara ya Maili sita na Rumu Lyamungo Nkuu mpaka Mkoa katika Jimbo la Hai na kwa sababu barabara hii inapata misukosuko hiyo hiyo ya hiyo barabara nyingine iliyozungumzwa mahali hapa.

Kwa maana kwamba inahudumia wakazi zaidi ya laki moja na iko katika miteremko mikali.

Je, kwa sababu barabara hizi vilevile ni fupi, kwa nini Serikali isiweke mpango maalum wa kuhudumia barabara hizi za sehemu za milimani ambazo zinasababisha ajali kubwa na wakati huo huo zinahudumia wananchi wengi mno hasa ikizingatiwa kwamba eneo la maporomoko ya mlima Kilimanjaro linaidadi kubwa ya watu kwa kilomita za mraba kuliko eneo lingine lolote la nchi na linapata sifa ya kuwa sehemu ya kijijini lakini ni mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA, (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai na Kiongozi wa Upinzani hapa Bungeni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni-*declare interest* kwamba huyu ni jirani yangu, *once upon a time* Siha ilikuwa ni sehemu ya Hai, hii barabara anayoizungumzia ninaifahamu, ni kweli iko katika haya matatizo yanayozungumza hapa. Mpango maalum

ambao naufahamu kwa sasa hivi ni kwamba, mipango yote hii sasa, yote tunajaribu kuiingiza sasa katika Bajeti *system* yetu, kwa maana ya kwamba tuweze kuitekeleza kwa kutumia. Mimi nakiri kwamba barabara hii inamatatizo kama ile nyingine iliyozungumzwa, utaratibu ambao tumekuwa nao, ni huu wa kuitaka Halmashauri, ilete maombi maalum.

*By mistake* kama haijafanyika hivyo, *it is too late*, kwa sababu sasa ndiyo uko kwenye mchakato wenyewe. Lakini mimi nashauri kwamba kama iko katika hali hiyo na wale wengine wote wanaozungumzwa, sasa tukimaliza hapo, Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwa sababu isije ikaja hapa wakanikaba tena koo, nataka niseme kwamba, tunapokwenda kwenye mpango maalum, inaweza ikapitishwa pale, ni sisi na Halmashautri husika tunaondoka hapa tunakwenda Hazina, Hazina na Mheshimiwa Mgimwa yuko hapo, tunafuata tena.

Sasa utaratibu umegeuka sasa unakwenda kwenye mipango kule, kwa maana ya *priorities*, kwa maana ya vipaumbele kulingana na hali yenyewe inayozungumzwa pale. Napenda kukiri kwamba barabara hii ina matatizo hayo. Tutashirikiana na Mheshimiwa Mbowe ili tuone tunasaidiaje barabara hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Haiwezekani kuzidi maswali hayo, kwa hiyo tunaendelea na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu.

Na. 2

**Wananchi Kupewa Hati za Kimila**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. SHAFFIN A. SUMAR)** aliuliza:-

Jimbo la Tabora Kaskazini lina maeneo makubwa ya mashamba lakini wananchi wa Jimbo hilo hawajanufaika na MKURABITA:-

(a) Je, lini wananchi hao watapewa Hati za Kimila na ni Kata zipi zipo kwenye mpango huo wa MKURABITA?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutambua Hati za Kimila ili wananchi waweze kukopesheka kwenye mabenki?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tshaffin A. Sumar Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Uyui, Baraza la Madiwani lilichagua vijiji vinne ambavyo ni Imalauduki, Kata ya Usagali, na Ufururuma, Kata ya Ufururuma katika Jimbo la Tabora Kaskazini. Vijiji vingine ni Miyenze, Kata ya Miyenze na Lutende Kata ya Lutende katika Jimbo la Igalula.

Mafunzo ya kujenga uwezo yamefanyika katika vijiji vya Lutende na Miyenze kuanzia tarehe 19 Novemba, 2012 mwaka jana mpaka tarehe 6 Januari, mwaka huu 2013 ambapo mashamba 1,054 yalipimwa na Hati 545 ziliandaliwa na zoezi la kuandaa Hatimiliki bado linaendelea. Mara tu utakapokamilika utaratibu wa utoaji Hati utafanyika.

Halmashauri ya Wilaya ya Uyui itaendelea na urasimishaji ardhi kwa vijiji hivyo viwili ambavyo ni Imarauduki katika Kata ya Usagali na Ufuruma katika Kata ya Ufuruma kuanzia mwezi Aprili, 2013. Mpango wa kurasimisha Wilaya yote ya Uyui itaandaliwa na utekelezaji wake utasimamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada ya Serikali kutambua Hatimiliki za Kimila ili wananchi waweze kukopesheka kwenye mabenki, Serikali kupitia MKURABITA imebuni na kuandaa maboresho katika Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Na. 5 ya mwaka 1999 kwa lengo la kuondoa ugumu

uliopo katika Sheria, unaofanya mabenki kusita kutambua Hatimiliki za Kimila. Mchakato wa mabadiliko hayo unaendelea, mara tu utakapokamilika mabadiliko yataletwa Bungeni ili kupata idhini ya Bunge. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, ningependa niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mfumo huu wa utoaji wa Hatimiliki za Kimila nchi nzima kumekuwa na matatizo, kwamba, zoezi hili kwanza linachukua muda mrefu, lakini pia zoezi lenyewe halitambuliki na halieleweki ipasavyo. Je, Serikali inachukua jitihada gani kuweza kuainisha maeneo yote yapimwe na kuweza kuwapa wananchi Hati hizi ili waweze kujikwamua kiuchumi?

Pili ni kwamba, hivi sasa tumeingia katika mgogoro mkubwa sana baina ya wananchi na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa nini sasa Serikali isiainishe hayo maeneo, ikawatambulisha wananchi fursa zilizopo, kulikoni kuwapa kipaumbele watu ambao wanasema wao ni wawekezaji, mara nyingine wanapewa Hati hata katika maeneo ambayo tayari yanamilikiwa na wananchi na inaleta migogoro? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSINO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mangungu, kama ifuatavyo:-

Kwanza, zoezi hili linachukua muda mrefu kwa sababu Halmashauri nyingi bado hazijalichangamkia kulifanyia kazi. MKURABITA kwa namna yoyote ile haiwezi kupima ardhi ya Tanzania nzima, lazima kazi hii ifanywe kama sehemu ya maendeleo ya eneo linalohusika. Kwa hiyo, MKURABITA inapokwenda katika wilaya inapima vijiji, inafundisha wapimaji na hasa vijana waliomaliza *form four*, inawapa vifaa vya upimaji, inaacha na hati pale.

Ni wajibu wa Halmashauri sasa kutengeneza utaratibu wa kuendeleza kutoka pale ili kazi hii iweze kufanyika kwa kasi zaidi badala ya kutegemea wapimaji kutoka Dar es Salaam kupima kila kijiji cha Tanzania. Kwa hiyo, katika eneo hili tukifuata utaratibu huo upimaji unaweza ukaenda kwa kasi zaidi.

Kuhusu migogoro ya ardhi na wawekezaji, hili ni jambo la utawala ambalo linahitaji kufanyiwa utaratibu mzuri. Kwanza kwa mujibu wa Sheria ya Vijiji, ardhi ya vijiji haistahili kupewa mtu yeyote bila kushirikisha hao wenye ardhi wenyewe. Kwa hiyo, kuwapatia Hati wawekezaji katika ardhi inayomilikiwa na vijiji bila kushirikisha vijiji vyenyewe ni kuanzisha mgogoro.

Jambo hili liliwahi kuzungumzwa katika Bunge hili na tulikwishatoa ahadi kwamba tutafanya uchunguzi ili maeneo ambayo yamefanyiwa makosa au kulikuwa na mgogoro wa ardhi yaweze kupatiwa ufumbuzi na tusiendelee kuwa na migogoro ya aina hii. *(Makofi)*

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Kwa kuwa dhana ya MKURABITA ni urasimishaji ardhi ili kuipa thamani, na kwa kuwa katika Bunge lililopita tuliazimia kuanzisha *EPZ* za vijana, sasa Serikali haioni ni wakati mwafaka wa kuanzisha maeneo maalum ya uzalishaji kwa vijana yenye Hati maalum? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSINO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kilimo chetu sasa hivi kinahusisha zaidi watu ambao ni wenye umri mkubwa, na kwamba vijana wengi bado hawashirikishwi kikamilifu katika sekta hii ambayo kusema kweli ndiyo nguvu kazi inayoweza kufanya kilimo kuwa endelevu.

Kwa hiyo, pamoja na kukubaliana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge kwamba ni vizuri tuwe na maeneo kwa ajili ya kilimo kwa vijana, lakini vijana ni wengi na pamoja na hayo ni lazima wawe sehemu ya vijiji ili unapopima na kutoa Hati, utoe vilevile kwa vijana.

Mimi nimekwenda katika Wilaya ya Ludewa na nikatoa Hati kwa wakulima na sehemu kubwa ya wale ambao walipewa hizo Hati walikuwa vijana. Kwa hiyo, huwezi kuwa na vijiji vya vijana na vijiji vya watu wengine. Mimi nadhani ardhi lazima ipimwe na itolewe kwa wote. Mahali ambapo kuna ardhi kubwa zaidi na vijana wanaweza waka- *settle*, wakafanya kilimo kikubwa zaidi ni jambo la busara kufanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Munde, pole na matatizo.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali imeishatoa Hati za kimila kwa baadhi ya wananchi, lakini Hati hizo zimekuwa hazitambuliki kwenye taasisi zetu za kifedha, benki na hatimaye wananchi hao kukataliwa kupewa mikopo na kuambiwa Hati hizi haziwezi kutumika katika mikopo.

Je, Serikali iko tayari sasa kukaa na taasisi hizi na benki ili kuweza kuwaambia wawape wananchi mikopo kwa kutumia Hati za Kimila? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSINO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Munde ningependa kumpa pole sana kwa kupotelewa na mama yake, Marehemu Mosi Tambwe, kifo ambacho kilitokea na tulipata habari hii kwa masikitiko makubwa.

Baada ya kueleza masikitiko hayo napenda kujibu swali lake kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumekuwepo na matatizo ya baadhi ya taasisi za fedha kutotambua Hati hizo, lakini taasisi nyingine zimekuwa zinatambua na mikopo imetolewa. Kwa hiyo, ili kuondoa mkanganyiko wa taasisi moja au nyingine kutambua au kutotambua ndiyo maana nimesema katika jibu la msingi kwamba yanaandaliwa mabadiliko ya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 ili tuweke kipengele ambacho kitafanya benki na taasisi nyingine zote kwa pamoja kutambua ili mikopo iweze kwenda kama ilivyokusudiwa.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, lakini kwa ridhaa yako naomba nijitambulishe kwanza kwa cheo changu kipya, *AKC 4513 Service Girl,* Mariam Kasembe. Baada ya hapo naomba swali langu Na. 3 lipatiwe majibu. (*Makofi*)

**SPIKA:** Itabidi wote mliopata majina mengine mumwandikie Spika, nawapongeza sana, nasikia mlifanya vizuri, kanyolewa na kipara. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 3

**Tatizo kubwa la Maji – Masasi**

**MHE. MARIAM R. KASEMBE** aliuliza:-

Jimbo la Masasi hasa vijijini kuna tatizo kubwa la maji hasa kwa sababu visima vilivyokuwa vimechimbwa havikutoa maji na Mheshimiwa Rais kwa kulitambua tatizo hilo alishauri kuchimba mabwawa ya maji katika kata mbalimbali ili kukabiliana na tatizo hilo kubwa:-

Je, Serikali imejiandaa kuchimba mabwawa mangapi katika bajeti ya 2012/2013?

Katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kuna ahadi ya kukarabati bwawa la Mchema na kuchimba bwawa jingine katika Mto Myesi.

Je, kazi hiyo inatarajiwa kuanza na kukamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli lipo tatizo la upatikanaji wa maji chini ya ardhi katika baadhi ya maeneo nchini ikiwa ni pamoja na maeneo ya vijijini katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Ili kuwapatia huduma ya maji wakazi wa maeneo hayo, Serikali hutumia vyanzo mbadala vya maji ikiwemo teknolojia ya mabwawa na uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba.

Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali kupitia mfuko wa TASAF na nguvu za wananchi imepanga kujenga mabwawa Kumi (10) katika vijiji vya Mraushi, Masonga, Maswela, Muungano, Mnazimmoja, Mchombe, Nankwanda, Chiwale, Nanjota na Kivukoni.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Serikali itafanya upembuzi yakinifu wa mabwawa matatu ya Lukuledi, Mihima na Namatutwe.

Mheshimiwa Spika, bwawa la Mchema lilijengwa mwaka 1949 kwa ajili ya kuhudumia wakazi wa mji wa Masasi. Bwawa hilo liliharibika mwaka 2002. Katika juhudi za kulikarabati bwawa hilo Serikali ilimwajiri Mtaalam Mshauri wa kufanya ukaguzi wa kimazingira na kijamii. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa:-

(i) wananchi wamepimiwa viwanja na kujenga kwenye eneo la kidaka maji *(intake ya maji)* pamoja na sehemu ya eneo la bwawa; na

(ii) mtiririko wa maji kwenda kwenye bwawa umezuiwa na tuta la barabara. Kutokana na matokeo hayo Mtaalam Mshauri amependekeza kuwa utafiti ufanyike kwa ajili ya ujenzi wa bwawa jipya kwenye mto Myesi. Fedha kwa ajili ya utafiti huo zimetengwa katika Bajeti ya mwaka 2013/2014.

Aidha, sambamba na kazi hiyo mradi wa maji wa Masasi – Nachingwea uko katika hatua za mwisho za kukamilika. Hivyo, wananchi wa Masasi Mjini watapata maji ya kutosha kutokana na mradi huo wa Masasi – Nachingwea ambao utekelezaji wake uko katika hatua za mwisho.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa napenda niishukuru Serikali kwa kuwa iko tayari kuchimba mabwawa Sita katika jimbo la Masasi, lakini vilevile kufanya upembuzi yakinifu wa mabwawa matatu. Nashukuru sana.

Kwa kuwa, bwawa hili la Mchema tayari fedha ziliishatengwa na kwa hivi sasa haitawezekana kuendeleza uchimbaji wa bwawa hilo kwa sababu tayari kuna watu waliopimiwa viwanja katika vidaka maji.

Je, fedha zilizokuwa zimetengwa kuchimba bwawa hilo na kwa kuwa jimbo langu la Masasi lote lina mahitaji ya mabwawa, haziwezi kupelekwa sehemu nyingine zikaendelea kuchimba mabwawa ili wananchi waweze kupata huduma ya maji?

Kwa kuwa, waliopima viwanja katika eneo la bwawa hili walikuwa wanatambua wazi kwamba eneo lile ni chanzo kikubwa cha maji kwa wananchi wa jimbo la Masasi.

Je, Serikali haiwezi kuwachukulia hatua kwa sababu wamefanya makusudi kupima viwanja kwa maslahi yao na hivi sasa wananchi wangu wa jimbo la Masasi watakuwa wanakosa huduma hii?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam R. Kasembe, kama ifuatavyo:-

Kwanza nipokee shukrani ambazo amezitoa kwa Wizara, na tunasema tutaendelea kuhakikisha maji yanapatikana maeneo mengi hapa nchini.

Swali la kwanza kuhusiana na fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la Mchemba zihamishiwe kwenye miradi mingine ya mabwawa katika halmashauri ya Masasi, ni kwamba Halmashauri ile ilikuwa na ahadi mbili.

Ahadi ya kwanza ilikuwa ni bwawa la Mchema na ahadi ya pili ilikuwa ni kuangalia utafiti wa bwawa la Myesi. Sasa baada ya kufanya upembuzi yakinifu na utafiti kuona kwamba bwawa hili haliwezi kuendelezwa, tutaelekeza nguvu kwenye bwawa la Myesi.

Kwa hiyo, fedha ambazo zilikuwa zimetengwa kwenye bwawa la Mchema ile nguvu itaelekezwa kwenye bwawa la Myesi ili kuona kwamba pale sasa tunapata bwawa jingine jipya kwa ajili ya mahitaji ya wananchi wa Masasi.

Swali la pili kuhusu kuwachukulia hatua wale ambao wamepima viwanja na kuwagawia wananchi, ni kwamba hili halitawezekana kwa sababu wakati viwanja hivi vinapimwa Sheria ya Maji ya mwaka 2009 ilikuwa haipo ambayo kama ingekuwepo ingekuwa ilieleza kwamba kile ni chanzo ambacho hakiruhusiwi watu kujenga na ingekuwa imekitangaza kwenye gazeti. *(Makofi)*

Sasa kama unazingatia huko nyuma ni kwamba hizo sheria hazikuwepo kwa hiyo ndiyo maana wale wakapima na kugawa vile viwanja. Lakini kuanzia sasa yale maeneo yote ambayo ni vyanzo vya maji, Wizara ya Maji inayatambua kwanza, inapima na ikiishapima inaweka kwenye sheria kwamba hairuhusiwi mtu yeyote kwenda kujenga pale. Kwa maana hiyo baada ya sheria ya mwaka 2009 kwa watu watakaokuwa wamevamia sehemu ambazo zimepimwa watatozwa na wanaweza wakachukuliwa hatua za sheria.

**SPIKA:** Askari mwingine Silinde!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, na mimi naitwa Afande *AG. 0587 Service Man, David Ernest Silinde. (Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji nchini limekuwa ni sugu na mwisho wake mpaka sasa hivi haujulikani. Kwa kuwa, tangu tupate uhuru kuna vijiji havijawahi kupatiwa mradi wowote wa Maji wa Serikali.

Je, Serikali inaweza kutueleza sababu ya kwanini baadhi ya vijiji havijawahi kupatiwa kabisa miradi ya Serikali ya maji kama ilivyo katika kijiji cha Mkonko jimboni kwangu pamoja na Usoche na maeneo mengine nchini. Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Silinde kama, ifuatavyo:- Kwanza nimpongeze kwa kumaliza mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea maendeleo tuna maana kwamba zipo changamoto ambazo zinatakiwa kutatuliwa. Naamini kwamba changamoto ndizo zinazoleta maendeleo, kama changamoto zisingekuwepo tusingekuwa na mipango. Tunaweka mipango kwa sababu changamoto zipo na tunatakiwa tuwachukue wananchi wetu kutoka mahali fulani kwenda mahali fulani.

Kwa hiyo, katika Wizara ya Maji, kama Wizara zingine tunao mpango ambao ni wa utekelezaji kupeleka maji vijijini na mijini na sehemu zingine katika makao makuu ya mikoa.

Hii ni *program* ya *WSDP* ambayo ni ya miaka mitano, mitano, ambayo ilianza na vijiji kumi (10) katika kila Halmashauri. Sasa viko vijiji ambavyo vimeishaanza kutekeleza na vimeanza kutoa matunda kama ninavyoongea sasa hivi karibu vijiji 67 katika vile vijiji vya Benki ya Dunia vimezinduliwa na vimeanza kutoa maji.

Kwa hiyo, hata vile vijiji ambavyo havijapata maji tutafika kwa sababu ni mchakato wa maendeleo na tumeuingiza kwenye mpango na tutavifikia vikiwemo vijiji vya Mheshimiwa Silinde. *(Makofi)*

Na. 4

**Uuzwaji wa Mashamba ya Wananchi kwa Wawekezaji**

**MHE. PAULINE P. GEKUL** aliuliza:-

Wananchi wanaoishi katika shamba la *Sigino Estate* Babati wametakiwa kuhama sehemu hizo japokuwa wameishi tangu Operesheni Vijiji mwaka 1974:-

(a) Je, kwa nini Serikali imeruhusu uuzaji wa mashamba hayo toka Mwekezaji wa zamani kwenda mwingine?

(b) Je, kwa nini Serikali haikugawa mashamba hayo kwa wananchi baada ya Mwekezaji wa awali kushindwa kuendeleza mashamba hayo badala yake yanauzwa kwa mwekezaji mwingine?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kutoa ufafanuzi kuwa jina sahihi la shamba linaloulizіwa na Mheshimiwa Mbunge ni Singu. Aidha, kumbukumbu zilizopo kwenye Daftari la Masijala ya Ardhi, Wizarani kwangu zinaonesha kuwa shamba la *Singu Estate* lililopo Wilayani Babati awali lilikuwa linamilikiwa na Hayati Lieutenant Richard F. Cooper, tangu mwaka 1930 kwa matumizi ya kilimo na ufugaji. Mmiliki alifariki mwaka 1952 na kufuatiwa na mkewe mwaka 1954 na hivyo shamba hilo kuwa chini ya uangalizi wa Mwanasheria wake ambaye alikuwa akiishi nchini Kenya. Baada ya mmiliki kufariki wananchi walikodisha shamba hilo kwa mikataba ya muda chini ya Mwanasheria wa marehemu.

Mwaka 1973 uongozi wa Serikali mkoani Arusha ulipendekeza kuwa umiliki wa shamba hilo ubatilishwe kutokana na ukiukwaji wa masharti ya matumizi ya ardhi. Tarehe 21 Desemba, 1978 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alibatilisha Hatimiliki ya shamba hilo na ubatilisho kuandikishwa tarehe 20 Februari, 1979. Mara baada ya shamba hilo kutwaliwa na Serikali vyama vya ushirika vya msingi vilialikwa kulipa fidia ya maendelezo yasiyohamishika kwa warithi wa mmiliki wa zamani lakini vyama hivyo vilikataa.

Mwaka 1982 Serikali iliridhia maombi ya Kampuni ya Bia Tanzania *(TBL)* ya kupatiwa eneo hilo kwa ajili ya kulima zao la shayiri. Kampuni hiyo ilipatiwa jumla ya ekari 3,113.5 na kusajiliwa kwa Hati Na. 11837 baada ya kulipa fidia ya shilingi milioni moja (1,000,000/=). Eneo lililobaki lenye ukubwa wa ekari 2,451 liligawiwa kwa wananchi wa vijiji vya Sigino, Dohom, Arri, Kiru, Dick na Daghailoy kwa ajili ya matumizi ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, *TBL* waliendelea kulima shamba hilo hadi mwaka 1995 ambapo wananchi walianza kuvamia pamoja na kujenga vibanda vya kuishi. Kampuni ilitumia muda mwingi mahakamani badala ya kuzalisha mazao yaliyotarajiwa. Mwaka 2011 Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya *TBL* iliuza shamba hilo kwa *Agric Volution* ambaye ni mwekezaji mwenye uzoefu wa muda mrefu katika kilimo cha shayiri kwa madhumuni ya kuwekeza ili kuboresha zao hilo.

Mwekezaji huyu tayari amekarabati majengo na miundombinu ya shamba hilo na anaendelea na kilimo ambapo mwaka huu amelima kiasi cha ekari 600 na eneo lililobaki amewaruhusu wananchi kulima. Aidha, kampuni hiyo imeandaa mpango mkakati wa namna watakavyoendeleza kupanua eneo watakalolima wao ili kutimiza lengo la kuzalisha zao la shayiri.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mchango wa wakulima wakubwa katika maendeleo ya uchumi wa taifa letu hususan katika uzalishaji wa mazao ya biashara. Kwa sababu hiyo Serikali haina mpango wa kufuta mashamba makubwa kwa lengo la kuwagawia wananchi mashamba hayo kwani kufanya hivyo kutakatisha tamaa wawekezaji.

Vilevile Serikali inaheshimu haki ya wananchi ikiwa ni pamoja na makampuni binafsi na ya umma kumiliki mali kama ilivyoelekezwa kwenye Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Hivyo kwa kuwa mmiliki wa shamba la Singu hakukiuka masharti ya umiliki kama yalivyoainishwa kwenye Hatimiliki iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

Serikali iliheshimu haki yake ya kuliuza bila kubadili matumizi ya ardhi kwa lengo la kuboresha uzalishaji badala ya kumnyang'anya na kuligawa kwa wananchi kama anavyopendekeza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Naibu Waziri amesema kwamba, Serikali inatambua mchango wa Wakulima Wakubwa na haiko tayari sasa kugawa lile Shamba kwa wale Wananchi wa Kata ya Sigino katika vijiji ambavyo vimetajwa. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

(i) Wakati *TBL* wakiuziana na Kampuni nyingine hii Wananchi hao walikuwepo na *TBL* alikuwa akikodisha Shamba hilo kwa Wananchi kwa muda wote na wakati analiuza alikuwa anajua kabisa kati ya eka 3113 ni eka 600 tu ambazo zinaendelezwa. Sasa naomba nifahamu Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wale Wananchi wanatulia wanalima kwa sababu sasa hawaruhusiwi kulima kabisa? Serikali ina mpango wa kuwapeleka wapi hao Wananchi?

(ii) Katika majibu inaelezwa kwamba *TBL* ilivyowauzia Kampuni ya *Agric Volution* kati ya eka 3,113 ni eka 600 ndiyo zinatumika na Mwekezaji huyu wa sasa anawapa Wananchi kwa hisani tu na wale Wananchi hususan wa Kijiji cha Singu ambao wapo miaka yote katika eneo hilo na wanafanya chaguzi na Mheshimiwa Naibu Waziri hakutaja hicho Kijiji ndiyo hao wanaopata hiyo adha. Napenda kufahamu kwa nini Serikali isimbakishie huyu Mwekezaji wa sasa hizi eka 600 tu na zile zilizobaki wapewe Wananchi hawa wakiwemo Wananchi wa Kijiji cha Singu ambao walikuwepo tangu mwaka 1974 lakini hadi leo hawatambuliwi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, majibu kwa kifupi kwa sababu hata *original* yalikuwa marefu mno.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi,

Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gekul kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Pauline Gekul, kwa jitihada zake anazofanya kuwasilisha maslahi ya Wananchi wa Mkoa wake anaowawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kwamba, Serikali ina mpango wa Wananchi wanaolima katika Shamba hilo. Katika jibu la swali la msingi nilieleza wazi kwamba, Serikali haina mpango wa kufuta mashamba makubwa kwa sababu tuelewe kwamba, Wakulima wakubwa wana uwezo kwa maana ya kuwa na teknolojia na hivyo wana uwezo wa kuzalisha kwa eneo kubwa kuliko Wakulima wadogo ambao wengi hulima kwa ajili ya kupata mahitaji yao binafsi, chakula cha kuwatosheleza wao na kidogo cha kuuza. Taifa linahitaji tuzalishe kwa wingi zaidi kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini na ziada kwa ajili ya kuuza nje.

Sasa Mwananchi yeyote kuingia kwenye shamba ambalo amemilikishwa Mwekezaji bila ridhaa yake, kama nilivyoeleza awali, *TBL* kwa muda mrefu walikuwa Mahakamani wakivutana na Wananchi hawa; lazima Wananchi waheshimu sheria, hatutaendekeza suala la kwamba kwa kuwa nimeshaingia ndani basi niache niendelee kuwepo kwa sababu huko ni kukiuka sheria. Lazima tulinde maslahi ya Wananchi wote kwa maana kama ni Mwekezaji; awe Mwananchi au awe ametoka nje, lazima maslahi yao yalindwe kwa mujibu wa sheria. Kwa maana hiyo ni kwamba, ninachowaomba Wananchi ambao wamevamia Shamba hili, waanze kuondoka wampishe Mwekezaji. Pale ambapo Mwekezaji anaona kwamba hataweza kulima eneo hili kwa mwaka husika, atawaruhusu walime, lakini pale ambapo atakuwa amejiimarisha sasa na kuendelea kulima aachiwe alime.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba, kwa nini Wananchi wa Singu wasibakizwe pale. Natumaini swali hili halipishani sana na lile la kwanza na ni ukweli kwamba, Serikali

haiingilii suala la umiliki wa Shamba lile kwa sababu mwenyewe ameshaonesha mpango wake wa kuliendeleza, ametuletea Mpango Kabambe kuonesha ni jinsi gani ataliendeleza Shamba lile na sisi kazi yetu ni kufuatilia. Pale ambapo itadhihirika wazi ameshindwa kuliendeleza, Serikali itatoa Shamba lile kwa mwekezaji mwingine.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba niseme ni kwamba, Serikali inatambua kuwa wapo baadhi ya Wawekezaji au Watu wanaojiita Wawekezaji, wanafika hapa nchini na wengine ni Watanzania, wanaomba ardhi kwa ajili ya kilimo, lakini baada ya muda mfupi wanaacha kulima walichotuambia watalima, badala yake wanaanza kugawa vipande vipande mashamba hayo na kuuza kwa Wananchi kama viwanja au vipande vidogo vidogo vya mashamba; hilo hatutalikubali. Tunashirikiana sasa hivi na Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba, tunalinda ardhi ya kilimo kwa sababu tunahitaji chakula, tunahitaji mazao ya biashara kwa ajili ya viwanda vyetu na kwa ajili ya kuuza nje.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mngekuwa mnajibu maswali namna hiyo, yangekuwa maswali matano tu kwa siku. Mheshimiwa Laizer, kwa kifupi.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wakati mwingine Serikali inapotoa ardhi ya vijiji kwa Wawekezaji wanaitoa bila makubaliano na waliopo katika maeneo hayo. Serikali haioni kwamba inapotumia ubabe huo inasababisha mgogoro kati ya Wananchi na Mwekezaji na kati ya Serikali na Wananchi; na je, ni lini Serikali itachukua utaratibu mzuri kuacha ubabe huo inaoufanya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Laizer, kama ifuatavyo:-

Kwanza, naomba tu nimwambie kwamba, Serikali haitumii ubabe wa namna yoyote ile, kwa hiyo, hilo tutasahihishana baadaye lakini ndiyo suala la msingi.

Kuhusu kwamba Serikali inagawa ardhi ya kijiji bila kuwashirikisha Wananchi, sheria ipo wazi; Sheria ya Ardhi ya Vijiji inasema, wenye mamlaka ya ardhi iliyo ndani ya kijiji kilichopimwa na kijiji kile kupatiwa Cheti cha Ardhi ya Kijiji, yapo kwa Wananchi wa Kijiji hicho. Ndiyo maana hata ukileta ombi la kumilikisha ekari moja kwamba naomba mnipe hatimiliki ya ardhi hii iwe kama *general land,* hatufanyi kazi hiyo mpaka tupate muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Kijiji, unaothibitisha kwamba Wanakijiji wote kwa pamoja wamekubali wewe umilikishwe ardhi ile. Huo ndiyo utaratibu wa kisheria ambao tunauzingatia.

Kwa bahati njema, Sheria inasema kwamba, mwenye mamlaka ya kuhaulisha ardhi iwe ni nusu eka au ni ekari moja kutoka Ardhi ya Kijiji kwenda kwenye Ardhi ya Ujumla, kwa maana *ya General Land* ni Rais wa Jamhuri ya Muungano pekee. Kwa hiyo, mwekezaji yeyote anapoleta ombi kwamba mimi nimepata ardhi kijiji fulani zipo taratibu inapitia kwenye Kamati ya Kugawa Ardhi ya Wilaya, ambao watahakiki kwamba hilo limefanyika, itakapokuja Wizarani tuna Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi, nao wanaketi na kutazama maombi yale kisha tunaenda kufanya uhakiki kwa sababu lazima tutoe *notice* ya kwamba ardhi ile inatakiwa kuchukuliwa.

Baada ya kutoa *notice* na kama pingamizi linakuwa halijatokea, ndipo tunawasilisha kwa Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, si kweli kwamba, Serikali inatumia ubabe kugawa ardhi ya vijiji.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Mheshimiwa Felix Mkosamali atauliza swali hilo.

Na. 5

**Mashirika ya Simu Kulipa *Corporate Tax***

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI** aliuliza:-

Mashirika ya Simu ya *TIGO, VODACOM, ZANTEL* na *AIRTEL* yamekuwa yakilipa *Corporate Tax* na Serikali haijafaidika na kodi nyingine:-

(a) Je, Kampuni hizo zimepata faida kiasi gani kwa kipindi cha miaka mitano, na Serikali imefaidika nini; hasa ikilitiwa maanani kuwa baadhi ya Kampuni hazijasajiliwa kwenye *Dar es Salaam Stock Exchange*?

(b) Je, Benki Kuu inasimamia vipi huduma za *M-Pesa, Tigo Pesa* na *Airtel Money* tangu zianze?

(c) Je, ni lini Kata za Murungu, Komsenga, Rugongwe, Mabaniba, Kizazi katika Jimbo la Muhambwe zitapatiwa minara ili waweze kupata mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu Tanzania iliporuhusu ushindani kwenye Sekta ya Mawasiliano, mchango wa Sekta hii katika uchumi na maendeleo ya nchi umekuwa mkubwa. Pamoja na kushuka kwa bei za huduma za mawasiliano mwaka hadi mwaka ukilinganisha na Sekta nyingine, makusanyo ya kodi yameongezeka sana. Kwa mfano, Ongezeko la Thamani (*VAT*), imekuwa ikiongezeka na kwa mwaka 2011/2012 pekee, Sekta ya Mawasiliano iliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 288 wakati makusanyo ya kodi hizo kupitia kinywaji cha bia ikiwa ni shilingi bilioni 270.

Kwa upande wa Kodi ya Kampuni (*Corporate Tax*), Makampuni ya Simu kwa ujumla wao katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, yamelipa jumla ya shilingi bilioni 64, huku jumla ya uwekezaji hadi kufikia mwaka 2010 ikiwa ni shilingi trilioni 2.563, sawa na ongezeko la asilimia 46 kwa mwaka. Kwa upande wa ajira, Sekta ya Mawasiliano imechangia ajira za moja kwa moja 1,934 na ajira zinazoibuliwa *(Indirect Employment)* kiasi cha 595,922.

(b) Mheshimiwa Spika, Benki Kuu husimamia huduma za *M-pesa, Tigo Pesa* na *Airtel Money* kwa kuhakikisha yafuatayo:-

(i) Benki Kuu hujiridhisha kwamba huduma inayotolewa inazingatia vigezo vyote vya mfumo ulio salama na wa uhakika kabla ya kutoa vibali vya huduma za kifedha kupitia simu za mkononi;

(ii) Ili kupata kibali, mwombaji hutakiwa kuwasilisha nyaraka mbalimbali zikiwemo nakala halisi za leseni zinazohusika kutoka Mamlaka ya Mawasiliano, Mkataba halisi wa Kisheria baina ya Kampuni ya Simu ya Mkononi na Benki ya Biashara ambayo itatunza fedha za wateja, nakala ya Mkataba kati ya Kampuni ya Simu na wateja wake ambao ndiyo watumiaji wa huduma hizo. Masuala mengine yanayowasilishwa na mwombaji ni pamoja na gharama zinazotarajiwa kutozwa kwa ajili ya huduma zitakazotolewa, mikakati iliyopo ya kupambana na kuzuia mizunguko ya fedha haramu na kulinda mtandao wa majanga yatokanayo na matumizi ya teknolojia sanjari na kubainisha teknolojia ya mtandao itakayotumika na namna huduma hizo zitakavyotolewa kitaalam; na

(iii) Kabla ya kibali kutolewa, Benki Kuu huhakikisha kuwa huduma za kifedha zinazotolewa na simu za mkononi, zinafuata Sheria na Kanuni zilizopo za Kifedha na Mwongozo wa Mfumo wa Malipo wa Kieletroniki (*Electronic Payments Guidelines*). Aidha, Kampuni ya Simu huwasilisha Benki Kuu taarifa za huduma kila mwezi.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia na kusimamia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi, Benki Kuu huhakiki fedha zilizopo kwenye mzunguko na zile zilizoko kwenye akaunti za dhamana. Aidha, Benki Kuu imeingia katika makubaliano maalum na Mamlaka ya Mawasilano (*TCRA*) ili kushirikiana katika kusimamia huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Benki Kuu ipo katika hatua za mwisho za kutayarisha Kanuni za Utoaji Huduma za Kifedha kupitia simu za mikononi ambapo zitatolewa leseni, badala ya vibali vya sasa, kwa kampuni zinazoendesha huduma hizo.

(c) Mheshimiwa Spika, kuhusu kupatiwa mawasiliano ya simu kwenye Kata za Murungu, Kumsenga, Rugongwe, Mabamba, Kizazi katika Jimbo la Muhambwe, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umefanya tathmini kujua mahitaji ya mawasiliano katika Kata hizo. Tathmini iliyofanyika katika maeneo ya Kata za Kizazi, Murungu na Rugongwe, inaonesha kuwepo kwa mawasiliano hafifu kutokana na hali ya milima na mabonde pamoja na kwamba kuna minara maeneo ya karibu. Pamoja na changamoto hizo, Serikali inaendelea na hatua za kuhakikisha kuwa wananchi wake wanapata mawasiliano. Hatua hizo ni pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kushirikiana na Kampuni za Simu ili kuangalia namna nzuri ya kuboresha mawasiliano katika Jimbo la Muhambwe.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Tumekuwa tunasuasua sana kwenye kukusanya kodi; kwa mfano, Kenya mwaka 2010 ilikusanya Dola za Kimarekani milioni 79, Uganda ilikusanya Dola za Kimarekani milioni 36, Rwanda ilikusanya Dola za Kimarekani milioni 14, Tanzania ilikusanya Dola za Kimarekani milioni 1.7 kwa mwaka 2010. Sasa tunazidiwa mara kumi na mbili na Rwanda, nchi ambayo Wananchi wake wanalingana na Wateja wa Vodacom pekee. Serikali inasema nini juu ya aibu

na fedheha ambayo mmekuwa mnaifanya kushindwa kukusanya kodi? *(Makofi*)

(ii) Kata hizi ambazo nimezisema katika Jimbo la Muhambwe zina zaidi ya Wananchi 150,000. Mfuko huu wa Mawasiliano kwa wote unatenga fedha kwenye bajeti ya mwaka huu au ya mwaka kesho ili Wananchi hawa waweze kupata mawasiliano. Zaidi ya Wananchi 150,0000 hawana mawasiliano kabisa wala siyo hafifu kama Naibu Waziri alivyosema. Kwenye bajeti ya mwaka huu, fedha za kufikisha mawasiliano kwa Wananchi hawa zipo au hazipo na Serikali ina mpango gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu kodi, kodi zipo za aina nyingi; kuna *VAT*, kuna *Import Duty*, kuna *Corporate Tax* na hizi kodi ukizijumlisha sina uhakika ni hizo ambazo ameziweka, lakini twende moja kwa moja kwenye nia ya Serikali kuhakikisha kwamba tunapata kodi nyingi zaidi au tunapata mapato mengi kutoka kwenye haya Mashirika ya Simu.

Serikali ina mpango wa kuweka *a monitoring system* ambayo itahakikisha kwamba, inaangalia matumizi ya simu zote, *data.* Inaangalia mazungumzo pamoja na *message* na mchakato wa kuhakikisha *system* hii inaanza umefika katika hatua nzuri sana. Manunuzi yamekwishafanyika, Mkataba umeshasainiwa, sasa hivi kilichobaki ni Kanuni ambazo zinasubiri kupitishwa na Wadau na Mheshimiwa Waziri atazisaini haraka iwezekanavyo ili tuweze kuwa na hiyo *system* mapema mwaka huu.

Kuhusu Kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kuwemo kwenye bajeti, itakumbukwa kwamba, tuna fedha kupitia Benki Kuu kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, hizo fedha zipo na ndiyo sababu tumetangaza *tender* na baadhi ya

maeneo tayari sasa hivi kuna wakandarasi wanajenga minara kwa ajili ya kuhakikisha Wananchi wanapata mawasiliano.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kwenye maswali hakuna utaratibu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mtu anadanganya unafanyaje?

**SPIKA:** Naomba tumalize, muda wetu ni *fixed*. Mheshimiwa Mbunge, muda wetu ni *fixed*, kwa hiyo, hatuwezi kuendelea na kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa tumekuwa tukishuhudia wizi mwingi na utapeli mkubwa unaofanyika kwa kutumia mitandao hii ya simu. Je, Serikali ina mpango gani kukabiliana na tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Catherine Magige, kama ifuatavyo:-

Mitandao ya simu ni sawa sawa na mitandao mingine yoyote inayohusu utumiaji wa pesa. Kwa mfano, tuna mitandao ya *ATM,* tuna mitandao ya simu za kawaida hizi za kwetu za *landline* na tuna mitandao ya simu za mkononi. Wajibu wa kwanza wa kuhakikisha fedha zako au kulinda fedha zako ni wa mteja mwenyewe. Kuna kitu kinaitwa *password* na hii *password* nirudie tena na kuwaomba

Wananchi, hiyo ni sawasawa na ufunguo wako wa kwenye *safe*. Tofauti iliyoko ni kwamba, ufunguo unakwenda unafungua kwenye *safe* yako. Huu ni ufunguo wa kwenda kwenye pesa zako ambazo zimewekwa kielektroniki, sasa usimpe mtu mwingine.

Nirudie tena, hata kama wewe ni baba usimpe mke wako, hata wewe mama usimpe mume wako ili uweze kujihakikishia kwamba pesa zako ni salama.

Na. 6

**Ahadi ya Kupeleka Umeme Tarafa ya Kibengu**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Tarafa ya Kibengu yenye Kata za Mpanda, Ihalimba na Kibengu na Vijiji 16 ndiyo chanzo kikuu cha Bwawa la Kihansi lenye uwezo wa kuzalisha megawati 180, lakini inasikitisha kuona kwamba Serikali imeshindwa kutekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme kwenye Vijiji vyote vya Tarafa hiyo:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake kwa kupeleka umeme kwenye maeneo hayo ambayo ni chimbuko la umeme wa Kihansi na kutoa huduma kama vile elimu, afya, barabara na kadhalika kwa Vijiji vya Ukeremi, Chongo, Uhafiwe, Ihimbo na Mapende vinavyozunguka Bwawa la Kihansi?

(b) Je, ni lini Waziri wa Nishati na Madini atakuwa tayari kuja kuzungumza na Wananchi wa Tarafa hiyo ili kupunguza jazba walizo nazo kwa kuona kuwa Serikali haiwatendei haki?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, lenye vipengele (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi Kabambe wa Awamu ya Pili wa Kusambaza Umeme Vijijini kupitia Wakala wa Serikali wa Nishati Vijijini *(REA)*, unahusisha Vijiji vya Ukami, Uhafiwe, Kipanga, Ihimbo, Mapende, Igeleke, Ilogombe, Chongo, Usokami, Ihalimba, Ihomasa na Ikongosi. Vijiji hivi ni pamoja na vile vilivyotajwa katika swali la msingi. Zabuni za Mradi huu zilifunguliwa mwezi Machi, 2013 ambapo mchakato wa kumpata mkandarasi wa kutekeleza Mradi uko katika hatua za mwisho. Makadirio ya gharama ya Mradi huo ni shilingi milioni 445. Mradi huu utaanza kutekelezwa wakati wowote ndani ya mwaka huu wa 2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutembelea Tarafa ya Kibengu, nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, nitatembelea Tarafa hiyo kadiri muda utakavyoniruhusu, lakini pia tutakavyowasiliana na Mheshimiwa Mbunge tuone ni namna gani tunaweza tukapata muda wa kwenda huko.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na yaliyojaa tija. Niulize swali moja la nyongeza.

Katika jibu la pili, amesema muda utakavyoruhusu. Mimi nataka *commitment* yake kwa sababu mwaka jana nilimwandikia barua na akanihakikishia kwamba angeweza kutembelea Tarafa ya Kibengu, lakini mwaka umepita hakutembelea na mwaka huu ananiambia kadiri muda utakavyoruhusu. Hajui kwamba kutembelea vijiji ni moja ya majukumu yake? Nataka atamke mbele ya Bunge lako Tukufu lini atatembelea Tarafa ya Kibengu?

**SPIKA:** Hilo tu, haya naomba utamke.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka jana nilipata fursa ya kutembelea Mikoa ya Iringa na Mbeya lakini sikuweza kufika kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Nirudie tu kusema tutapanga mimi na yeye tuone lini tunaweza tukaenda ndani ya kipindi hiki cha Bunge.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Katika mpango wa kupeleka umeme Wilaya ya Mufindi ikiwemo Kata ya Malangali, Serikali ilishaahidi na ilishatenga shilingi bilioni 1.9 na iliahidiwa kwamba, utekelezaji huo unaanza mwaka huu na Wananchi walishafanya *wiring* katika nyumba zao. Sasa Wananchi wa Malangali wanauliza ni lini kazi ya kuweka nguzo na kusambaza umeme itaanza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mendrad Kigola, kama ifuatavyo:-

Kweli nilitembelea Jimbo la Mheshimiwa Mbunge na kwa bahati mbaya sikufika Malangali, lakini Mbunge tulioanana naye na mara kadhaa anapouliza swali lake majibu yamekuwa ni haya. Niseme tu kwa Wabunge wote kwamba, zaidi ya vijiji 1000 vipo katika huu utaratibu wa mchakato wa manunuzi ambao tunatarajia kuukamilisha wakati wowote na ndiyo hiyo Miradi ambayo tutaikamilisha katika kipindi cha mwaka huu huu wa 2013. Nichukue nafasi hii kumwomba sana Mheshimiwa Mbunge, awatoe wasiwasi watu wa Malangali ikiwemo na Sekondari ya Malangali, kwa sababu najua kuna tija na ahadi kubwa ambayo tuliitoa kule kama Serikali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, ukiangalia Wabunge wengi malalamiko yao ni utekelezaji wa Miradi ya Umeme Vijijini na ukiangalia kwa mwaka jana tulipitisha bajeti kwa ajili ya kuhakikisha umeme unafika katika vijiji na

malalamiko ya Wabunge mpaka hivi sasa maeneo mengi bado Miradi haijaanza. Sasa tunaenda mwaka mwingine wa Bajeti na tayari muda mrefu umepita, bado hizo fedha hazijapelekwa kwa ajili ya kuanza Mradi na kuna fununu kwamba *REA* hakuna fedha. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na Miradi ambayo tayari ilishapitishwa na kuelekea bajeti ijayo kwa ajili ya utekelezaji?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, kama ifuatavyo:-

Kweli utakumbuka kwamba, katika Bajeti iliyopita tulikuwa na vijiji zaidi ya 1000 ambavyo tulikuwa tumedhamiria na dhamira yetu bado iko vilevile kwamba, tutatekeleza na tutavipatia umeme ndani ya mwaka huu wa fedha.

Mchakato wa manunuzi ndiyo tumefungua hizo *tender* mwezi Machi, hivi majuzi tu, na kwa hiyo tunaweza tuka-*award* wakati wowote kuanzia sasa. Naomba sana Waheshimiwa Wabunge, mvute subira kwa sababu ni kweli na ni uhakika kwamba, Miradi hii kama ambavyo tulikuwa tumeahidi katika bajeti iliyopita, lazima itatekelezwa kwanza kabla ya kuanza Miradi mingine mipya.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, wakati wa bajeti maswali ni saa moja tu na imeshapita. Tuendelee na swali lingine ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Kamani.

Na. 7

**Hospitali ya Kijiji cha Mkula Kupatiwa Umeme wa Gridi**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Hospitali ya AIC Mkula ambayo sasa imependekezwa kuwa Hospitali Teule ya Wilaya mpya ya Busega haina

Umeme wa Gridi wakati kuna nyaya za umeme zimepita kijijini hapo kuelekea Bariadi:-

(a) Je, Serikali itafunga lini umeme wa grid katika hosptali hiyo?

(b) Je, tatizo gani limekuwa likikwamisha utekelezaji wa mpango huo kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mbunge wa Busega, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Kazi za kufunga Umeme wa Grid ya Taifa kwenye Hospitali ya AIC Mkula ambayo imependekezwa kuwa Hospitali Teule ya Wilaya mpya ya Busega, zimejumuishwa katika Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ya Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).* Kazi hizo zitajumuisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilomita mbili, njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita tatu, ufungaji wa transfoma moja yenye KVA 200 na kuunganishia umeme wateja zaidi ya 509. Gharama za kazi zote zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 143. Zabuni ya kuwapata wakandarasi ilitangazwa mwezi Desemba, 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, 2013. Kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote ndani ya mwaka huu wa 2013.

(b) Mpango huo haukuweza kutekelezwa mapema kutokana na maandalizi ya Mradi pamoja na taratibu za ununuzi kuchukua muda mrefu.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Mradi huu ninaouzungumzia nyaya zilifungwa tangu mwaka juzi na umeme ukawashwa katika vijiji vilivyoko Wilaya ya Bariadi na kuruka vijiji viwili tu ikiwemo hiyo Hospitali ya Mkula katika Wilaya ya Busega. Je, hii haileti sura ya ubaguzi wa Serikali katika kuhudumia Wananchi wake?

(ii) Majibu haya ya Naibu Waziri yanafanana na majibu aliyonipatia mwaka jana nilipouliza juu ya kufuatilia Miradi ya Umeme katika Wilaya ya Busega na sasa ni mwaka mzima umepita tangu majibu hayo niyapate na hakuna kazi iliyofanyika. Vivyohivyo kwa Miradi mingine ya Umeme katika Jimbo hilo ukiwemo Mradi wa Nasa – Nyamikoma na Nasa – Ngasamo. Nimefanya utafiti pia Miradi hii inayotekelezwa na Symbion karibu nchi nzima inasuasua. Sasa ni namna gani Naibu Waziri atanihakikishia kwamba Wananchi wa Busega watapata umeme katika Miradi hii iliyoainishwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, kama ifuatavyo:-

Kweli kwamba siku za nyuma wakati walipokuwa wana-*design* utekelezaji wa Miradi hii ilikuwa kama Mradi unaelekea sehemu fulani kwa kulenga vijiji Fulani, basi wanapeleka moja kwa moja kwenye vijiji vile hata kama viko vingine pembeni kidogo kwa umbali wa kilomita moja. Tumejaribu kukubaliana sisi Wizarani na tumeshawaeleza wenzetu wa *TANESCO* na *REA* kwamba, katika *design* za Miradi yote sasa hairuhusiwi kuruka kijiji, lakini pia kijiji kilicho pembeni kidogo, umbali wa kama kilomita moja, unasema kwa sababu *line* yako inakwenda kule kwenye kijiji fulani unakiacha, pia nayo haina tija kwa sababu umeme huu tunazungumza habari ya uchumi katika suala la umeme.

Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, hili jambo halitarudia na vijiji hivi viwili anavyovisema ikiwa ni pamoja na chenye hospitali, ni kweli vilirukwa na tumeviingiza katika Programu yetu ya Miradi tutakayoitekeleza sasa.

Suala la pili kwamba majibu haya ambayo nimeyatoa leo yanafanana; ni kweli yanafanana kwa sababu hata swali linafanana na lililopita.

Sasa pamoja na hivyo, nichukue nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli Miradi inayotekelezwa na Symbion hasa ile ya *MCC* imesuasua maeneo mengi. Nimekwenda Mbeya na Iringa, tumezungumza nao tumekubaliana kwamba, wafanye kila wanaloweza wahakikishe hadi mwezi Juni mwaka huu wawe wamemaliza Miradi hiyo. Vinginevyo, kwa kweli inatuletea matatizo sana kwa sababu ni kweli kazi zimefanyika nusu halafu wanapotea wanakaa muda mrefu, lakini tumeshalizungumza na tumeshaliweka sawa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, Miradi hii itatekelezwa, hadi ifikapo Juni, Miradi yote ya *MCC* itakuwa imekamilika.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Tatizo ambalo linajitokeza Busega kwa maana ya nyaya kupita katika maeneo mbalimbali linajitokeza pia katika Miji ya Kasulu na Kibondo ambako tunatumia umeme wa jenereta. Ukiangalia jenereta hizi, kwa mfano, Mji wa Kasulu zinazalisha umeme wa megawati 2.5 na hata 0.5 ile bado haijatumika yote, jambo ambalo linasababisha *TANESCO* kutumia gharama kubwa kuendesha jenereta hizo.

Naomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge lako Tukufu ni lini Serikali itachukua hatua zaidi kwa maana ya kuimarisha suala zima la kufanya usambazaji wa umeme ili kupunguza gharama za uendeshaji ambazo zinalikabili Shirika la *TANESCO* na Wananchi waweze kupata umeme kama ambavyo imekusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Moses Machali, kama ifuatavyo:-

Kweli tulikuwa na Miradi iliyopita katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwemo Kasulu na Kibondo lakini sasa Miradi ile ilikuwa ina wigo wake kwamba imefika hapo ndiyo hapo. Hata kama kuna nyumba mbili zinaendelea huko lakini Mradi huo kwa maana ya kazi hiyo ilikuwa inaishia mahala fulani basi watamalizia hapo na tutakuja na Mradi mwingine ili tuweze kuendelea kwa sehemu ambazo zimebaki. Ndiyo maana utaona Mheshimiwa Machali, amekuwa akiuliza sana hili na jibu lake litawezekana pale ambapo tutatekeleza hii Miradi ambayo tuliipanga sasa kuitekeleza ambayo maeneo ya vijiji hivyo ambavyo vimeachwa na Mradi uliopita sasa tutaviingiza katika utekelezaji wa Miradi hii. Isiishie hapo, aje tuweze kuona ni namna gani tutafanya kama havitakuwepo katika orodha ya vijiji vilivyoko sasa kwenye Mpango huo wa *REA.*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Vituo vya Afya vilivyoko kwenye Tarafa za pembezoni mwa Wilaya vinafanya kazi sawa na Hospitali Teule za Wilaya; kwa mfano, Kituo cha Afya cha Mgongo na kule Tarafa ya Igurubi Wilayani Igunga pamoja na kule Nduguti Wilaya mpya ya Mkalama na viko kwenye ahadi za mara nyingi Viongozi wanapopita. Je, ni lini Vituo vya Afya vya aina hii ambavyo viko mbali na Hospitali za Wilaya vitapatiwa umeme ili Wananchi waweze kupata huduma za matibabu?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Madelu, kama ifuatavyo:-

Kwanza, nampongeza Mheshimiwa Mbunge, amejaribu kuzungumzia Majimbo ambayo ni ya Wabunge wengine na hii kwa kweli inafanya kazi ya kizalendo sana; hongera sana Mheshimiwa Nchemba. Ni kweli tunazo programu ambazo tunafikiria kwamba ni vyema Vituo vya Afya na maeneo ya pembezoni ni lazima tuweze kuyapatia umeme; na hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Miradi hii ya *REA* tunayotaka kuitekeleza sasa,

tumezingatia sana hilo. Kwa vile maeneo aliyoyataja yamo katika hii Miradi, tukitoka hapa tuwasiliane niweze kumwonesha namna tulivyoipanga na kandarasi zinakaa namna gani katika zile *lots* ambazo tumeziuza na tunategemea kupata wakandarasi wakati wowote kuanzia sasa.

Na. 8

**Mradi wa Majaribio wa MKUHUMI**

**MHE. ALI KHAMIS SEIF** aliuliza:-

Hivi sasa hapa nchini kuna Mradi wa MKUHUMI *(REDD)*:-

(a) Je, maeneo gani yapo kwenye Mradi huo?

(b) Je, majaribio hayo yamefanikiwa kwa kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mradi wa Majaribio wa MKUHUMI unatekelezwa Tanzania Visiwani (Unguja katika Shehia 25 kwenye Wilaya za Kusini Unguja, Kati na Kaskazini B na Pemba katika Shehia 15 kwenye Wilaya za Mkoa wa Pemba, Chakechake, Wete na Micheweni) na Tanzania Bara katika Wilaya za Kilolo, Kondoa, Uvinza, Kilosa, Lindi Vijijini, Rungwe, Sumbawanga, Kahama, Shinyanga Vijijini, Kisarawe, Ilala na Kilwa). Maeneo mengine ni kwenye Misitu ya Mikoko, Misitu ya Ukanda wa Pwani na Misitu yote ya Tao la Mashariki.

(b) Mafanikio ya Mradi wa Majaribio wa MKUHUMI ni kama ifuatavyo:-

(i) Wananchi wanaendelea kuhamasika kutunza misitu kwa lengo la kufaidika na rasilimali za misitu na kupata motisha ya kifedha kwa kuuza hewa ukaa.

(ii) Mkakati wa Kitaifa wa MKUHUMI umekamilika na kuidhinishwa na Serikali. Uandaaji wa Mkakati huu umehusisha wadau mbalimbali wakiwemo baadhi ya Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

(iii) Vijiji vimeweza kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ambayo itawezesha vijiji kupata Cheti cha Kusimamia Ardhi ya Kijiji.

(iv) Mchakato wa kuanzisha Chuo cha Kitaifa cha Hewa ya Ukaa *(National Carbon Monitoring Center),* unaendelea kwa ufadhili wa Serikali ya Norway; na Andiko la Mradi huu lipo tayari, majadiliano na Serikali ya Norway kupitia Ubalozi wao hapa nchini yapo katika hatua za mwisho.

(v) Mafunzo na tafiti za mabadiliko ya nchi ikiwemo MKUHUMI yanaendelea katika baadhi ya Vyuo Vikuu hapa Nchini, ikiwemo Mamlaka ya Hewa Tanzania, wanafunzi 17 wako katika Programu za *Ph.D.* na 50 katika ngazi za sayansi ya uzamili hapa nchini na kwingineko.

(vi) Sita, takwimu za upimaji wa misitu nchi nzima *(National Forest Resources Monitoring and Assessment)* zimeshakamilika na kuanza kukokotolewa. Takwimu hizi zinatengeneza msingi wa kuweza kufuatilia, kutoa taarifa mbalimbali Kitaifa na Kimataifa na Ukaguzi wa kiwango wa hewa ya ukaa kilichopo katika misitu yetu.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zitatuwezesha kuingia katika soko la hewa ukaa na kuweza kunufaisha nchi na Wananchi watakaoshiriki katika MKUHUMI.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo ya nyongeza.

(i) Mradi huu upo katika majaribio na upo katika ufadhili wa fedha kutoka nchi za nje. Je, ufadhili huu utakapokuwa umekamilika Serikali imejipanga vipi kuuendeleza Mradi huu?

(ii) Taasisi gani ambazo zinaratibu Mradi huu wa MKUHUMI kwa sehemu ya Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ali Khamis Seif, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mradi huu upo katika majaribio na ningeomba niseme kuwa, tarehe 20 Machi, 2013, baada ya Mheshimiwa Waziri Kagasheki kufanya mazungumzo ya kina na Waziri mwenzake wa Norway, alinituma nishiriki katika ufunguzi wa Kituo kilichoko pale *SUA.* Ninaomba nimhakikishie kuwa, Serikali ipo katika hatua za juu kabisa katika uwezekano wa kutekeleza na ni kweli kabisa kuwa unategemea sana ufadhili wa fedha za nje.

Mikakati ya Serikali ya Tanzania imeifanya chini ya Mpango huu tunahakikishiwa na wadau wa maendeleo kuwa tutakuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa, ufadhili na fedha za kufadhili Miradi hii nchini kote zitakuwepo.

La pili, kwa hivi sasa kama nilivyosema katika jibu la msingi, Kituo cha *SUA,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na baadhi ya wadau wengine muhimu nchini, wanashiriki kama sehemu ya majaribio elimishaji na tuna uhakika kabisa kuwa tunaweza kupanua wigo wa Mradi huu nchini kote.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio mazuri ya Mradi huu na mikakati mizuri ya Serikali, nilitaka kujua ni lini Serikali itatanua wigo ili kuhakikisha maeneo mengine ya nchi yanafaidika na zoezi hili.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali na kama tulivyosema, upanuzi wa uwigo huu utasaidia sana kwa sisi kama nchi kupata fursa ya kupata fedha zinazotokana na biashara hii ya hali ya hewa ili tuweze kufaidisha Wananchi wetu na pia tuweze kutoa motisha kwa utunzaji wa mazingira. Kazi kubwa hapa ni ya Wananchi ambao zaidi ya asilimia 95 wanatumia mkaa, wanatumia kuni, waweze kupata motisha na mbadala ili waweze kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi gesi joto inachangia zaidi ya asilimia 20 ya kuharibu uoto huu ulioko angani, ni matumaini ya Serikali kuwa tutapanua wigo katika misitu yetu yote nchini ikiwa ni pamoja na Tanzania Visiwani.

**SPIKA:** Mheshimiwa, ninaomba radhi muda umekwisha. Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, swali la mwisho.

Na. 9

**Vivutio vya Utalii Nchini**

**MHE. ANNE K. MALECELA** aliuliza:-

Nchi ya Tanzania ni ya pili Duniani kwa kuwa na vivutio asili vya utalii baada ya Brazili ambayo ndiyo inayoongoza Duniani:-

(a) Je, vivutio hivyo vilivyopo Tanzania ni vipi?

(b) Je, kila kivutio kinaliingizia Taifa mapato kiasi gani kwa mwaka?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio mbalimbali vya asili, ikiwa ni pamoja na milima na safu za milima mbalimbali ikiwemo Safu ya Tao la Mashariki, Maziwa yenye sifa, Miji ya kihistoria, Michoro ya Mapangoni, Tamaduni mbalimbali, Hifadhi za Taifa (15), Bonde la Hifadhi ya Ngorongoro, Mapori ya Akiba (28), Mapori Tengefu (44), yenye wanyama na ndege wa kuvutia, uzuri wa asili wa fukwe za bahari na maeneo ya ikolojia ikiwemo misitu ya asili na maeneo ya ardhi oevu, ambavyo kwa pamoja vinafanya Nchi ya Tanzania kuwa ya kipekee na kuvutia Watalii kutoka sehemu mbalimbali Duniani. Aidha, Tanzania ina maeneo saba yaliyotengwa na *UNESCO* kama Maeneo ya Urithi wa Dunia ambapo baadhi ya vivutio hivyo vya asili vimejumuishwa katika orodha ya maeneo hayo. Vivutio hivyo ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Mlima Kilimanjaro, Bonde la Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi mbili za Maeneo Tengefu ya Bahari *(Marine Reserves).*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, mwaka 2011, Watalii takriban 867,994 waliotembelea vivutio mbalimbali hapa nchini, waliliingizia Taifa Dola za Kimarekani bilioni 1.36, sawa na shilingi bilioni 2,107.61. Mapato hayo yaliingia kwenye Uchumi wa Taifa kutokana na matumizi ya Watalii katika kulipia huduma mbalimbali na ununuzi wa bidhaa mbalimbali na vito hapa nchini.

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaomba niishukuru Serikali kwa kutoa picha kamili kwa Watanzania ni kiasi gani nchi yetu ina utajiri mkubwa wa rasilimali.

Baada ya hapo, ninaomnba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kikatiba jukumu la kulinda rasilimali ya nchi yetu pamoja na utajiri wake ni la Serikali. Je, Serikali kupitia Bunge hili inaweza kuwaambia Watanzania inatekeleza jukumu hili kikamilifu?

(ii) Swali la pili; kama jibu ni ndiyo inakuwaje rasilimali zetu zinaibiwa, zinatoroshwa mara kwa mara kupitia kwenye viwanja vya ndege mfano ile ndege iliyotubebea wanyama wetu kupitia Kiwanja cha Kilimanjaro; Serikali inaweza kusema nini? Je, mnalinda rasilimali za Watanzania au mnakuwa ni sehemu ya kuifanya nchi hii iwe maskini?

Ninaomba tupate majibu mazuri kwa sababu Watanzania wanasubiri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa ni wajibu wa Serikali kama ilivyoainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za nchi na ni kweli kuwa kama alivyosema Mheshimiwa Mama Malecela, tumekuwa katika wakati wa tahadhari na wakati ambao ni mgumu kwa maliasili, siyo tu nchini bali kokote Duniani, kutokana na wingi wa Mtandao wa Kimataifa unaoendelea na hapa ninazungumzia suala la ujangiri wa wananyamapori na hasa ujangiri wa tembo.

Ijulikane kuwa, Tanzania kwa kutumia wenyeji wake katika Mitandao ya Kimataifa, ikiwa ni pamoja na *INTERPOL* pamoja na habari ambazo zimesema kuwa Wanyama walitoroshwa katika Uwanja wa Kilimanjaro au kwingine kokote, tumeweza kwa kushirikiana na Serikali zingine Duniani, kuwakamata hawa wahalifu wa Kimataifa katika Maziwa Makuu au katika maeneo wanayofikia kwa maana ya *port of entry* katika nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kufanya jitihada za dhati kushirikiana na washirika wetu wa Kimataifa ikiwa ni pamoja na majirani zetu wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki na Nchi za *SADC* ili tuweze kuhakikisha kuwa moja, tunakomesha kabisa ujangiri nchini. Pili, Serikali imepiga marufuku biashara zingine za kupeleka nje ya nchi Wanyamapori na tunahakikisha kuwa wahusika wote ambao walihusika hapo zamani wanachukuliwa hatua zote stahili za Kisheria na wale ambao wanaweza wakawa na mashaka juu ya azma ya Serikali, ninaomba kuchukua nafasi hii

kuwatahadharisha kuwa mtu yeyote ambaye hapo nyumbani kwake anafikiria kwenda kufanya ujangiri, anatafakari kuungana na mwenzake kwenda kuifanyia hila Jamhuri hii, tutamkamata na kumtia katika Vyombo vya Dola.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda umekwisha, si mnaona kwanza nimechukua muda ambao sikutakiwa karibu nusu saa nzima maana ni saa moja, wakati wa vipindi vya bajeti maswali ni saa moja.

Ninawakaribisha wageni wote mlioko hapa, lakini nimeanza kutangaza matangazo ambayo yanahusu vikao vya ujumla kusudi wale Wenyeviti walioleta maombi kwa ajili ya shughuli za Kamati zao waangalie namna watakavyoweza ku-*adjust* ratiba zao.

Kwa hiyo, leo baada ya kipindi hiki cha maswali, Kamati ya Kanuni za Bunge itakuwa na kikao saa tano katika Ukumbi wa Spika, halafu Kamati ya Uongozi maana ni Wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu, itakuwa na Kikao saa saba kamili mchana katika Ukumbi wa Spika. Baada ya hapo tutakuwa na Kikao cha *Briefing* cha Wabunge wote. Hiki ni kikao cha kawaida, kabla ya kuanza vikao vyetu huwa tunakuwa na kikao hicho na kitafanyika Ukumbi wa Pius Msekwa, saa tisa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, saa tano Kamati ya Kanuni, saa saba Kamati ya Uongozi na saa tisa Mkutano wa *Briefing* kwa Wabunge wote. Kama muda utaruhusu, Vyama vya Siasa vitakuwa na muda wa kukutana baada ya *briefing* kwa wote. Baada ya kusema hayo, Wenyeviti mta-*adjust* ratiba zenu kufuatana na haya matangazo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kuwa, saa tano asubuhi, kutakuwa na Kikao cha Kamati kujadili Taarifa za Kamati; na hawa watakutana Namba 227 na watakutana saa tano.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, anawatangazia Wajumbe wa Kamati yake kuwa, leo saa nane mchana, watakutana katika Ukumbi Namba 219. Kwa hiyo, m-*note* kuwa kuna Kamati ya Uongozi na vitu vingine, lakini tangazo ndiyo hilo.

Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Nyambari Nyangwine, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yao kuwa, leo saa tano asubuhi, kutakuwa na kikao katika Ukumbi Namba 23.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, Mheshimiwa Diana Chilolo, anaomba niwatangazie Wajumbe wake kuwa, saa saba mchana, watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Msekwa B. Ninaomba mwangalie *time.*

Mheshimiwa David Silinde, Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa CHADEMA kuwa, kutakuwa na Kikao cha Wabunge hao, saa saba mchana, katika Ofisi ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Kama nilivyosema, wote mta-*adjust time* kufuatana na matangazo ya awali.

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na haya niliyoyatangaza na kwamba bado tunajipanga vizuri kusudi kesho Mheshimiwa Waziri Mkuu, aweze kuingia na kutoa Hotuba yake, ninapenda kuahirisha Kikao cha Bunge mpaka hapo kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.04 asubuhi Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 10 Aprili, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*